EVANGECUBE®

UNFOLDING THE ANSWER TO LIFE'S GREATEST PUZZLE!

Vipi ya kuongoza muntu kwa Bwana Yesu

(Use the arrows on the cube to help you see how to open the pictures!)

1

Binadamu ametengwa na Mungu kwa sababu ya dhambi

- Hii nuru(onyesha upande wa kuliya) inamwakilisha Mungu
- Mungu yu kamili bila dhambi
- Mungu anatupenda sana!
- Mungu hataki tupotee, lakini anatamani tuwe na uzima wa milele pamoja naye.
- Lakini dhambi zetu lazima ziondorewe ili tuwe na uzima wa milele pamoja naye.
- Iyi picha (onesha upande wa kushoto) iko muntu kama wewe na mimi.
- Gizani iyi inawonesha dhambi zetu
- Dhambi ni kitu chochote tunachofanya tulichokataza na Mungu natuambia tuwacane
- Biblia inasema, "kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu. " (Warumi 3:23)
- Dhambi zetu zinatutenganisha na Mungu.

2



Fungua upande wa pili: "Kristo Msalabani"

- Mungu alitupenda sana hata akamtoa mwanawake pekee Yesu Kristo aje ulimwengu kamabinadamu.
- Yesu alipokufa msalabani alizichukua dhambi zetu yeye mwenyewe na kutulipia deni ya dhambi zetu." Yeye mwenyewe alizicukua dhambi zetu katika mwili wake juu ya mti ili kutika wafu kwa mambo ya dhambi tuwe hai kwa mambo ya haki; na kwa kupigwa kwake mliponywa. Kwa maana Kristo naye aliteswa mara moja kwa ajili ya dhambi, mwenye haki, kwa ajili yao wasio haki,ili atulete kwa Mungu; mwili wake akauawa, bali roho yake akahuishwa." (1 Petro 2:24, 3:18)
- Biblia inasema, " Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele" (Yohana 3:16) Biblia inasema ,"Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi." (Waromi 5:8)

3

Fungua upande wa Tatu "Kristo Kaburini"

- Watu walimzika Yesu kaburini
- Wakaliviringisha jiwe kubwa mbele yake.
- Askari wa kirumi wakalinda kaburi

4



Fungua upande wa Nne "Kufufuka kwa Yesu"

- Mungu baba alimutuma malaika aliviringishe mbali lile jiwe kubwa na kuwafukuzia mbali wale askari.
- Mungu alimfufua Yesu kutoka katika wafu!
- Baadaye kidogo Mungu alimchukua tena Yesu kwenda Mbinguni.
- Hii inaonyesha kwa hakika kwamba malipo ya yesu kwa dhambi zetu yalimtosheleza mungu na ya kwamba Yesu ameshinda dhambi, Shetani, na mauti!

5

Upande wa Tano:

- Yesu ndiye letu pekee lakwenda kwa Mungu"
- Yesu ndiye njia ya pekee ya kutufikisha kwa Mungu.Baba Mbinguni
- Yesu alisema katika Biblia:"Mimi ndimi njia,na kweli, na uzima. Mtu haji kwa Baba , ila kwa njia ya mimi" (Yohana 14:6)
- Kupitia Yesu, na kwa yeye pekee, tunaweza kusamehewa dhambi zetu zote na kupata uzima wa milele pamoja na mumgu milele.
- Lakini kujua tu kuhusu mambo haya haitoshi, lazima tuchague kuweka imani yetu katika Yesu-kumwamini yeye atuokoe kutoka dhambini.
- Pasipo kumwamini Yesu dhambi zako haziondolewi! (Waebrania 4:2)

6

Fungua kwenye "Mbingu na Kuzimu"

- Biblia inasema kwamba amwakiliye Yesu yuna uzima wa milele na hatahukumiwa. Lakini asiyemwamini Yesu tayari amekwisha hukumiwa na ghadhabu ya Mungu inamkalia (Yohana 3:16,18,36)
- Mshahara wa dhambi ni mauti bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu.
- Utachagua namna gani?
- Utamwamini Yesu aliyekufa ili akulipie dhambi zako, nakupokea msamaha na uzima wa milele? (Onyesha "Mbinguni")
- Au utamkataa Yesu Kristo na kuteseka kwa kutengwa na Mungu kwa adhabu ya dhambi zakoJehanum? (Onyesha "Kuzimu")

ULIZA SWALI

Je, Ugipenda kujua kwamba dhambi zako zimesamehewa na kwamba umepokea zawadi wa milele?

(Akijibu Ndiyo, Enderea)

Biblia inasema ,:" Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana utaokoka" Warumi:10:9 Ni naweza kukuongoza katika sala sasa hivi. Kumbuka, siyo maneno maalumu ambayo yatakuokoa. Mungu anaangalia moyoni mwako ili kuona imani ya kweli katika Yesu.Unaweza kumwamini Yesu hata sasa hivi kwa kuomba nami…Je, uko tayari?… Haya na tuombe…

Sala ya imani:

"Mungu, asante kwa kunipenda mimi./Ninaamini kwamba nimekutenda dahambi./Naamani kwamba mwanao, Yesu/ alikufa msalabani/ Kunilipia dhambi zangu/ Na kwamba ulimfufua katika wafu./Sasa naiweka imani yangu katika Yesu pekee /Unisamehe / Na uniokoe kutoka katika dhambi zangu./ Ninakiri kwamba Yesu ni Bwana!/ Asante kwa zawadi yako ya uzima wa milele./ Ninaomba katika jina la Yesu,/ Amina."

Hakika ya Wokovu



Onyesha "Mbinguni na Kuzimu"

- Kama umechukua hatua hiyo ya kumwamini Yesu Kristo hivi ndivyo Biblia isemavyo kuhusu wewe; "Bali wote waliompokea aliwapata uwezo uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake!" **(Yohana 1:12)**
- (Onyesha kwenye mikono) Yesu anasema, "Kondoo wangu waisikia sauti yangu, nami nawajua nao wanifuata; Nami nawapa uzima wa milele wala hakuna mtu atayewapokonya katika mkono wangu!" **(Yohana 10: 27-28)**

Onyesha "Daraja ya Kuvuka"

- Pia Yesu alisema, " Amini, amini nawaambia, Yeye alisikiaye neno langu na kumwamini Yeye aliyenipeleka yuna uzima wa milele, wala haingii hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia uzimani." (peleka kidole chako juu ya" Daraja la Kuvuka"…

Yohana 5:24

Rudi nyuma ,fungua upande wa "Mbinguni na Kaburi"

Kufanya Wanafunzi

7

Kumpenda Mungu kwa moyo wako wote, kumpenda jirani yako kama nafsi yako.

"Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote.Hii ndiyo amri iliyo kuu, tena ni ya kwanza. Ni ya pili yafanana nayo, ni hii, Mpende jirani yako kama nafsi yako."
Mathayo 22:36-40

Kujifunza Biblia kila siku.
Ukianzia na Injili ya Yohana, soma sura moja kila siku. "Kama watoto wachanga waliozaliwa, sasa yatamanini maziwa ya akili yasiyogoshiwa ili kwa hayo mpate kuukulia wakovu" **Petro 2:2**

Kuomba bila kukoma
Katika kuomba unaweza kumtukuza Mungu, kumwomba akusaidie, kuungama dhambi zako na kuwaombea wengine, "Msijisumbue kwa neno lolote, bali katika kila neno kwa kusali na kuomba pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu, na hekima ya Mungu ipityo akili zote itawahifadhi mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu." **Wafilipi 4:6-7**

Kukusanyika mara kwa mara pamoja na wakristo wengine
Mungu ameamuru kwamba Wakristo wakutane mara kwa mara kwa kuabudu, kuomba, kujifunza Biblia, na kusaidiana… "Wala tusiache kukusanyika pamoja kama ilivyo desturi ya wengine, bali tuonyane…" **Waebrania 10:25**

Tuwaelezee watu wengine Habali Njema ya Yesu Kristo
Mungu anataka tuwaelezee watu wengine jinsi ya kupata uzima wa milele pamoja na Mungu kwa kumwamini Yesu ili awaokowe kutoka dhambini. Unaweza kuchukua kifaa kama hiki, na kwenda kuwashuhudia watu " Yesu akawaambia, Enendeni mwote mkaihubiri injili kwa kila kiumbi." **Marko 16:15**

www.evangecube.org

Please give us your testimony: **testimony@evangecube.org**

EVANGECUBE INTERNATIONAL

Come use the EvangeCube to win people to Christ on a 1-week world missions trip with Global Missions Fellowship, Inc. Call 1-800-5-I-CAN-GO today! http:\\www.gmf.org

For more information contact:

EvangeCube International • 317 Main Street–Suite 207 • Franklin, Tennessee 37064

8 8 8 - 3 5 4 - 9 4 1 1

©2000 EvangeCube International